

Je, unaanza shule ya msingi?

Kuanza shule ni wakati wa kuisimua kwa watoto, wazazi pamoja na walezi. Mwaka wa kwanza wa shule ya msingi unaitwa Msingi au Maandalizi. Ili kujiandikisha katika shule ya msingi ya serikali ya Victoria, fuata hatua hizi mwaka mmoja kabla ya mtoto wako kuanza shule.

Kabla ya kujaza maombi

Soma kuhusu wakati na jinsi ya kujiandikisha kwenye tovuti yetu



Hakikisha mtoto wako ana umri sahihi wa kuanza shule



Tafuta shule ya eneo lako na nyingine za serikali zilizo karibu kwenye findmyschool.vic.gov.au



Wasiliana na shule za msingi ili kuweka miadi ya ziara, matembezi au kwa habari zaidi



Kuomba kujiandikisha kwenye Msingi (Foundation)

Chukua fomu ya maombi kutoka kwenye shule ya msingi



Kusanya hati zinazohitajika



Wasilisha kila kitu kwenye shule ya msingi kufikia tarehe iliyopangwa (Ijumaa ya mwisho ya mwezi Julai)



Subiri shule iwasiliane nawe (wiki 2 za kwanza za mwezi Agosti)



Unaweza kupata maelezo zaidi, na kufikia nyenzo zilizotafsiriwa, kwenye:

Kujiandikisha katika Msingi (Maandalizi) | Serikali ya Victoria



Department of Education